**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## BENKI KUU YA TANZANIA

**21 Machi 2025**

### TAARIFA KWA UMMA

### MABORESHO YA UWEKAJI WA BEI KWENYE MINADA YA HATI FUNGANI ZA SERIKALI

Benki Kuu ya Tanzania, kama wakala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inapenda kuufahamisha umma na wawekezaji kuhusu kuimarisha uwazi wa uwekaji wa bei katika minada ya hati fungani za Serikali.

Kwa sasa, wawekezaji huainisha kiasi cha uwekezaji na bei ya ushindani wanapowasilisha maombi ya kushiriki katika minada ya hati fungani. Hatahivyo, utaratibu huu hauonyeshi mchanganuo wa bei ikiwemo riba limbikizi na bei ya ujumla kwa minada ya hati fungani zinazotolewa kwa mara ya pili au zaidi.

Ili kuongeza uwazi katika uwekaji wa bei, kuanzia tarehe 2 Aprili 2025, wawekezaji watatakiwa kuainisha bei safi, riba limbikizi, na bei ya ujumla katika minada ya hati fungani. Riba limbikizi itatangazwa katika wito wa kushiriki katika mnada utakaotolewa wiki moja kabla ya mnada husika. Benki Kuu itaendelea kutumia kigezo cha bei safi katika kuchambua na kutoa matokeo ya mnada.

Fomu mpya ya maombi ya kushiriki kwenye minada inapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania (www.bot.go.tz). Fomu ya mfano imeambatanishwa kwa ajili ya ufafanuzi zaidi. Kwa maelezo zaidi wasiliana na wakala wa uwekezaji katika dhamana za serikali au Benki Kuu ya Tanzania.

**Emmanuel M. Tutuba**
**GAVANA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501

CDS/FOMU/03

# FOMU YA MAOMBI YA KUWEKEZA KWENYE DHAMANA ZA SERIKALI

**Jina la Wakala wa Uwekezaji:** XYZ BENKI/WAKALA WA SOKO LA HISA LA DSM

**Akaunti Namba ya Uwekezaji (CDS A/C):** BOTCDSXYZ0034

**Jina la Akaunti**: MADEMBWETA BYINO MBAGA

**Meneja Masoko ya Ndani**
**Benki Kuu ya Tanzania**
**2 Mtaa wa Mirambo**
**S.L.P 2939**
**11884 Dar es Salaam**
**Tanzania**

**Tarehe:** 15 DESEMBA 2024

**Aina ya Dhamana:** HATIFUNGANI

**Mtoaji (Issuer):** SERIKALI YA TANZANIA

**Tarehe ya Mnada:** 18 DESEMBA 2024

**Muda wa Kuiva:** MIAKA 20

Mimi/Sisi tunawasilisha maombi ya kushiriki kwenye Dhamana za Serikali kwa vigezo vifuatavyo:

| Na. | Kiasi cha Uwekezaji | Bei katika Nafasi Nne za Desimali | | |
|---|---|---|---|---|
| | Shilingi za Kitanzania | Bei Safi[1] | Riba Limbikizi[2] | Bei ya Ujumla[3] |
| 1. | 1,000,000/= | 100.0121 | 1.8883 | 101.9004 |
| 2. | 10,000,000/= | 99.0100 | 1.8883 | 100.8983 |
| 3. | 60,000,000/= | 100.0000 | 1.8883 | 101.8883 |
| 4. | | | | |

Kulingana na masharti ya wito wa kushiriki katika minada ya Serikali, Mimi/Sisi tunakubali kulipa kupitia "TISS-DVP" jumla ya kiasi nitakachoshinda katika bei ya ujumla.

15 DESEMBA 2024 M.B.M

**Tarehe** **Sahili** **Sahihi**

[1] Kwa **dirisha lisilo la ushindana**, Bei Safi itakua bei ya wastani (WAP). Kwa Dhamana za Serikali za Muda Mfupi Bei Safi itajazwa kwa msingi ya bei pungufu ya 100 (Discount Price).

[2] **Riba Limbikizi** ni riba ambayo mwekezaji atapokea katika tarehe iliyopangwa bila kujali kipindi alichokaa na hatifungani. Husika. Inapatikana katika wito wa kushiriki kwenye mnada. Hatifungani zitolewazo kwa mara ya kwanza hazitakua na riba limbikizi.

[3] **Bei ya Ujumla** = Bei Safi + Riba Limbikizi.